

Ilisishwa Mara ya Mwisho Februari 2024

Je, Unatimiza Masharti imeendelezwa

yako ni watu 10, unapaswa kuongeza **\$1345** nyingine zaidi ili kupata kiwango cha \$0 hadi \$15,870. Na kuendelea.

Je, Unahitaji Usaidizi wa Kubaini ikiwa Unatimiza Masharti?

Hakuna tatizo—tunaweza kukusaidia! Fuata tu hatua zilizo hapa chini.

Hatua ya 1

Hatua ya kwanza ni kujua ukubwa wa kaya yako. **Ukubwa wa kaya** ni idadi ya watu wanaoishi nawe.

Hali ya 1

Ikiwa una umri wa miaka **18 au zaidi**, kaya yako inaweza kujumuisha watu hawa—

Wewe

Mume/mke wako

Wategemezi wako. Huyu anaweza kuwa mtoto au jamaa ambaye unadai kuwa ni mtegemezi katika fomu zako za kodi. Katika mipango hii miwili, mtegemezi lazima awe anaishi nawe ili kuhesabiwa kama sehemu ya kaya yako. Mtegemezi ni mtu unayemtunza na kukimu mahitaji yake ya kifedha—unalipia chakula, nyumba, nguo na masomo yake, kwa mfano.

Kuna masharti maalum ambayo hukuruhusu kudai kuwa mtu ni mtegemezi. Ikiwa una maswali kuhusu iwapo mtu katika kaya yako ni mtegemezi au la, tafadhali tujulishe.

Kwa mfano, tuchukulie kwamba unaishi na mume/mke wako na watoto 2. Hiyo inamaanisha kuwa kuna watu 4 katika kaya yako. Ukubwa wa kaya yako ni 4.

Hali ya 2


Ikiwa una umri wa **chini ya miaka 18**, kaya yako inaweza kujumuisha watu hawa—

Wewe

Wazazi au walezi wako

Ikiwa wazazi au walezi wako wana **wategemezi**, unapaswa kuwahesabu pia. Inaweza kuwa ndugu (kaka au dada) au jamaa mwingine anayeishi nawe pia.

Kwa mfano, tuchukulie kwamba unaishi na mama na baba yako na kaka yako mdogo. Kaka yako ni mtegemezi wa wazazi wako. Kwa hivyo, unahitaji kumhesabu kaka yako pamoja na wewe na mama na baba yako. Ukubwa wa kaya yako ni 4.



Hatua ya 2

